**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

# TAARIFA KWA UMMA

## MAJUMUISHO YA ZOEZI LA UDAHILI WA WANAFUNZI WA NGAZI YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA MWAKA WA MASOMO 2025/2026 NA MAELEKEZO MAHSUSI KWA VYUO NA WANAFUNZI

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) liliratibu udahili wa wanafunzi kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa mwaka wa masomo 2025/2026 kuanzia tarehe 28 Mei, 2025. Zoezi la udahili lilikamilika tarehe 28 Oktoba, 2025.

### 1. UDAHILI WA WANAFUNZI KWA KOZI ZA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI

Maombi kwa kozi za afya na sayansi shirikishi kwa Tanzania Bara yalifanyika kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (CAS) na kwa upande wa Zanzibar maombi yalifanyika moja kwa moja vyuoni.

Jumla ya waombaji 49,148 walituma maombi ya kujiunga na vyuo katika programu mbalimbali. Waombaji 39,553 sawa na asilimia 80% ya waombaji wote walichaguliwa ambapo kati yao wanawake ni 20,131 sawa na 51% na wanaume ni 19,422 sawa na asilimia 49%.

### 2. UDAHILI WA WANAFUNZI KWA KOZI ZISIZO ZA AFYA

Maombi kwa kozi zisizo za afya yalitumwa moja kwa moja vyuoni na kisha vyuo viliwasilisha majina ya wanafunzi waliochaguliwa NACTVET kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki.

Jumla ya wanafunzi 108,109 waliochaguliwa na vyuo waliwasilishwa NACTVET kwa uhakiki wa sifa zao ambapo kati yao 106,022 sawa na asilimia 98% ya waombaji wote walikua na sifa za kujiunga na kozi/programu walizoomba.

### 3. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UDAHILI

i. Baadhi ya vyuo kuchagua waombaji wasio na sifa stahiki. Hii ni kwa baadhi ya vyuo visivyotumia Mfumo wa Udahili wa Pamoja(CAS).
ii. Vyuo kuwasilisha maombi ya udahili kwa niaba ya waombaji bila ridhaa yao, au kutumia namba za simu ambazo si za waombaji husika.

### 4. HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA BARAZA

i. Baraza kutoa fursa ya marekebisho kwa waombaji kuomba programu wanazokidhi sifa stahiki.Fursa hii ipo wazi hadi tarehe 30 Novemba, 2025.
ii. Elimu kwa wanafunzi juu ya umakini katika utunzaji na utoaji wa taarifa zao.

## 5. KUFUNGULIWA KWA VYUO

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitangaza kufunguliwa kwa vyuo vyote nchini kwa awamu mbili kama ifuatavyo:

Wanafunzi wa mwaka wa kwanza watawasili vyuoni kuanzia tarehe 17 Novemba, 2025 na wanafunzi wanaoendelea na masomo watawasili vyuoni kuanzia tarehe 24 Novemba, 2025

## 6. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA VYUO NA WANAFUNZI WALIODAHILIWA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026 NA WALE WANAOENDELEA NA MASOMO

### A. VYUO:

I. Vyuo vinasisitizwa kuwasajili wanafunzi wote waliochaguliwa na kufika vyuoni ndani ya muda uliopangwa (tarehe 17 Novemba, 2025 hadi 12 Desemba, 2025)
II. Vyuo kutopokea wanafunzi ambao hawakuchaguliwa kwenye vyuo husika.
III. Vyuo kutosajili mwanafunzi ambae hajafika chuoni.

### B. WANAFUNZI:

I. Wanafunzi wanatakiwa kuwasili katika vyuo walivyochaguliwa na kujisajili ndani ya muda uliopangwa.
II. Baada ya mwanafunzi kusajiliwa na chuo chake, aingie katika tovuti ya NACTVET (www.nactvet.go.tz), kuthibitisha usajili wake na kuhakiki taarifa zake kwa kubofya"link" inayosomeka "**student's information verification**". Iwapo mwanafunzi atathibitisha kutokuwepo taarifa zake sahihi, atoe taarifa chuoni kwake na pia NACTVET kupitia mawasiliano ya Baraza.
III. Wanafunzi wanaoendelea na masomo wanatakiwa kuhakikisha wamesajiliwa kwenye mfumo wa NACTVET na taarifa zao ikiwemo chuo, program na matokeo ya muhula husika ni sahihi na endapo taarifa zao si sahihi wawasiliane na vyuo vyao pamoja na kutoa taarifa NACTVET.

## 7. DAWATI MAALUM LA USAIDIZI KIPINDI CHA USAJILI

Baraza limeandaa dawati maalum kwa ajili ya kutoa usaidizi kwa wanafunzi na vyuo katika kipindi chote cha usajili wa wanafunzi vyuoni.

**Mawasiliano**
Namba ya bure: **0800110388**
WhatsApp: **0736 310 311**
Barua pepe: **info@nactvet.go.tz**
Mitandao ya kijamii ya NACTVET: **Facebook, Twitter na Instagram**

Baraza linatoa rai kwa vyuo na wanafunzi kufuata taratibu na miongozo ya Baraza. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote watakaokiuka taratibu na miongozo hiyo.

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MTENDAJI**

**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)**
**17/11/2025**